

Fid Q (Fareed Kubanda) – Propaganda

Uchambuzi *na* Bahati Mabala na Steven Nyabero @ <http://vijana.fm/>

[Kiitikio]

Polisi *wanasapoti* gangsta rap; “Ili uhalifu uongezeke.”
Wabana pua kuimba mapenzi; “Je, itafanya ukimwi usepe?”
Media *zinapromoti beef*; “Wanadai zinakuza muziki.”
Wadau wana wasanii wabovu; “Nye wakali mtatoka vipi?”
Hizi ni PROPAGANDA. Usiulize ni nani? Ni yupi? Saa ngapi? Ilikuwa? Na
nani? Ili iweje?
Hizi ni PROPAGANDA. Utaibiwa ukicheza ‘blanda’. “Yule [ni] *last King of
Scotland* sio Idi Amin wa Uganda!”

[Ubeti wa kwanza]

Machungu unapozimwa, ili ufunikwe na asiyeweza,
Mbaya zaidi wanampa promo, halafu kwenye show nammeza.
Hautaki kuwa tatizo sababu unaweza tatuka,
Hauwezi jua wapi nitatua ka’ jiwe gizani likitupwa.
Wanaficha ili nisione wakati tayari nishajua,
Hamkomi? Igeni nione jinsi msamba mnaupasua!
Hivi mnaishi ili mle au mnakula ili muishi?
Kumbuka, a small leak will sink a ship.
Mazingira hatarishi, mabwana afya wana mapesa mob;
Uswazi tunaomba mvua zinyeshe ili tutapishe vyoo.
Ogopa kuoja haraka kama unaogopa talaka.
Na *uki-vote in a hurry*, ujue *una-produce corruption*.
Maneno yao ni matamu, lakini midomo yao inanuka.
Ukipewa usisahau, ukitoa toa bila kukumbuka.
Usihofie kupitwa ilimradi muda haukuachi,
Amini kesho itafika kama ipo ili uipate.
Tunachukiana kwa sababu tunaogopana,
Tunaogopana kwa sababu hatujajuana,
Hatujuani kwa sababu tunatengana,
Dunia ni nzuri, walimwengu hawana maana!

[Kiitikio]

[Ubeti wa pili]

Polisi huniita mzururaji, na wanajua mie ni Mc,
Kisha hunipa ishara kama wanavuta uradi kwa Tasbih.
Baya lisilonidhuru ni jema li' so na faida.
Nashukuru kote nasikika napotoa haya mawaidha,
Kuanzia kata, tarafa, wilaya, mikoa hadi ngazi ya Taifa.
Nikifa siachi skendo, nina uhakika nitaacha pengo;
Kwa hivi vina hata wakulima hujikuta wanameza Mbegu.
Pia ni kama *liberation struggle* machoni mwa 'Chegu'.
Ukiwa mkali ka' Marco Chali... raia *wata-feel* tu.
Wajinga nd'o hufa kwa wivu sababu hawako *real* tu.
Rafiki sio urafiki usipochanganywa na kazi,
Mlango sio mlango hadi ufungwe au uachwe wazi,
Haupaswi kumuamini muongo hata kama akiongea ukweli.
Ni dhambi kutumia dini kama njia ya kututapeli;
Wanajiingizia kipato kwa kivuli cha misaada.
Hawatufunzi tuwe viongozi, labda viongozi wa kuwafuata;
Utata huja, tunapoanza kuwachunguza,
Badala ya kuwafuata, ndipo siri zinapovuja.
Tunajenga tabia kisha tabia zinatujenga;
Ukishindwa kujiendesha ujue mwenyewe tu ulipenda.
Kama umevutiwa na asali, jiandae kumkwepa nyuki;
Hauwezi kumtisha kwa mawe adui aliyeshika bunduki!
Ni uchunguzi tu wa kisayansi ambao haukufanikiwa,
kama ule wa ng'ombe kula nyasi tu halafu anatoa maziwa!

[Kiitikio]